iv. Kuendeleza matumizi ya haki za binadamu na uendelevu kama kigezo cha tuzo za sekta na biashara na mashirika ya biashara

c) Uchunguzi wa Kina wa Haki za Binadamu: serikali inapaswa kufanya iwe sharti kwa biashara kutambua athari zao za haki za binadamu ikijumuisha kupitia kuendesha tathmini tondoti na zinazoaminika za haki za binadamu kabla ya kuanza shughuli zao na kuendelea kuhakiki tathmini hizi ili kuhakikisha zinazuia, kushughulikia na kutatua ukiukaji wa haki za binadamu. Tathmini kama hizo za athari zinapaswa kuhusisha ushauriano wa maana na makundi ambayo huenda yakaathiriwa na washikadau wengine na kujumuisha athari mahususi

d) Kuripoti: Serikali inapaswa kutekeleza hitaji la biashara kuandaa ripoti za kifedha kulingana na Sheria ya Kampuni ya 2015 na kuhimizia ufichuzi wa athari zao kwa haki za binadamu na hatua za suluhu zinazochukuliwa kuhusiana na hili

e) Kushirikiana kwa uwezo wa kufikia suluhu: Serikali zinapaswa kufanya iwe sharti kwa biashara kushirikiana na mashirika ya serikali na washikadau wengine katika kuwezesha suluhu kwa ukiukaji wa haki za binadamu unaohusiana na biashara. Hizi zinajumuisha kuendelea kushiriki katika majadiliano ya sera kuhusu kufikia suluhu na kutekeleza sera zinazowezesha ufikiaji wa suluhu.

### Nguzo ya 3: Ufikiaji wa Suluhu

Uwezo wa kufikia suluhu inayofaa unawahakikishia waathiriwa wa dhuluma za haki za binadamu zinazohusiana na biashara njia zinazotabirika za kutoa malalamiko, kuendeshwa kwa kesi za malalamiko yao, fursa ya wahusika wengine kuwasilisha kesi zao na suluhu ya usawa kulingana na sifa za kesi husika. Pia inahakikisha kwamba suluhu zinafaa na zinawiana na dhuluma, ikijumuisha maagizo ya kukomesha dhuluma zinazoendelea.

### Suluhu za Serikali Zinazotokana na Mahakama na Zisizo za Mahakama

#### Hatua za Sera

Serikali:

a) Itatekeleza sheria zote zinazotumika na vilevile kuheshimu sheria na viwango vinavyotambuliwa kimataifa vya haki za binadamu kama vinavyohusiana na ufikiaji na ununuzi wa ardhi na maliasili, mazingira na usimamizi wa mapato

b) Itahimiza matumizi ya mbinu Mbadala za Utatuzi wa Mizozo katika kushughulikia mizozo kati ya biashara na wale ambao wanatuhumiwa kudhurika kutokana na shughuli za biashara hizo

c) Itatoa mafunzo na msaada kwa asasi za mahakama, utawala na usimamizi kuhusu wajibu wa biashara kuhusiana na haki za binadamu. Taasisi zifuatazo zitapewa kipaumbele:
   - ★ Taasisi ya Mafunzo ya Mahakama
   - ★ Kamati muhimu za usimamizi za bunge
   - ★ Mashirika muhimu ya udhibiti
   - ★ Biashara Muhimu Zinazomilikiwa na Serikali (SOE)
   - ★ Asasi za Kikatiba ikijumuisha KNCHR
   - ★ Kituo cha Upatanisho wa Kimataifa cha Nairobi
   - ★ Chama cha Wanasheria nchini Kenya

d) Itaboresha uwezo wa kufikia taarifa kuhusu mbinu zinazopatikana za mahakama na zisizo za mahakama zinazohusika katika utatuzi wa dhuluma zinazohusiana na biashara kama hatua ya kuendeleza ufikiaji wa haki. Taarifa kama hiyo inapaswa kufanywa ipatekane katika kaunti zote na kutolewa kwa njia inayoweza kufikiwa na makundi yote yaliyo hatarini

e) Itatoa kipaumbele kwa ufikiaji wa msaada wa kisheria kwa waathiriwa wa dhuluma za haki za binadamu zinazohusiana na biashara, kulingana na Sheria ya Msaada wa Kisheria ya 2016 na Mpango wa Hatua wa Kitaifa kuhusu Msaada wa Kisheria

f) Itaboresha ufikiaji wa Kitengo cha haki za binadamu cha Mahakama ya Juu. Mahakama ya Ajira na Leba na Mahakama ya Mazingira na Ardhi ili kuhakikisha kwamba ni njia zinazoweza kufikiwa za kusuluhisha dhuluma za haki za binadamu zinazohusiana na biashara. Uhakiki huu utajumuisha tathmini ya iwapo mahakama zinaendesha kesi haraka na gharama zao ni nafuu

g) Itaongeza uwezo wa idara ya uchunguzi wa leba ili kushughulikia malalamiko yanayohusiana na leba, ikijumuisha kupitia:
   - ★ Kuongeza idadi ya maafisa wa ukaguzi wa leba ili kufuatilia na kutekeleza utiifu wa viwango vya leba na biashara mbalimbali, huku maanani yakitiliwa katika utekelezaji wa sera za lazima ili kuzuia na kushughulikia unyanyasaji na dhuluma ya kingono, malipo ya mshahara wa kiwango cha chini zaidi, malipo sawa kwa kazi sawa kwa thamani sawa, kuzuia leba kwa watoto na kutokuwepo kwa ubaguzi dhidi ya wanawake, makundi yaliyotengwa na makundi ya watu walio wachache.
   - ★ Kuchukua hatua za kutoa uhakikisho wa uhuru wa maafisa wa ukaguzi wa leba na kuhakikisha kwamba majukumu yao yanafanywa kwa uadilifu na kwa njia ya uwazi na uwajibikaji.

### Mbinu za Malalamiko Zisizo za Serikali

Biashara zinapaswa kutoa mbinu za kushughulikia malalamiko ima kwa njia pekee kama mbinu za kiwango cha utendakazi, au kwa ushirikiano na washikadau au mashirika katika sekta kama sehemu ya mbinu zozote za kushughulikia malalamiko za sekta pana. Hii inanuiwa kuhakikisha suluhu ya haraka, inayoweza kufikiwa moja kwa moja na kifedha kwa malalamiko ya haki za binadamu.

Hatua za Sera

Serikali:

a) Itaunda na kusambaza mwongozo kwa biashara kuhusu kuunda mbinu za kuaminika za kushughulikia malalamiko ya utendakazi ambazo zinaambatana na viwango vya kimataifa. Mbinu kama hizo za kushughulikia malalamiko zinafaa kukidhi mahitaji na haki za makundi yaliyo hatarini kama vile wanawake, watu wanaoishi na ulemavu, watoto na watu asili.

b) Itahamasisha biashara na zile zilizoathiriwa na shughuli zao kuhusu manufaa ya kuunda na kutumia mbinu ya kuaminika ya kushughulikia malalamiko katika kiwango cha utendakazi.

c) Itasaidia mashirika ya kijamii yanayoshughulikia masuala ya haki za binadamu kukuza uwezo wao wa kufuatilia kwa ufanisi athari za haki za binadamu zinazoletwa na biashara mbalimbali na kurai watu binafsi na jamii kutekeleza haki yao ya kupata suluhu kwa ukiukaji wa haki za binadamu.

## 4. Utekelezaji na Ufuatiliaji

Utekelezaji wa sera hii utafanywa na Kamati ya Utekelezaji ya NAP itakayosimamiwa na Idara ya Haki na Tume ya Kitaifa ya Kenya kuhusu Haki za Binadamu. Washikadau kutoka sekta mbalimbali watakuwa wanachama. Washikadau hao ni:

1) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Idara ya Haki
2) Wizara ya Masuala ya Kigeni
3) Wizara ya Leba na Ulinzi wa Kijamii
4) Wizara ya Huduma ya Umma na Jinsia (Idara ya Serikali ya Jinsia)
5) Wizara ya Biashara na Viwanda
6) Tume ya Kitaifa Haki za Binadamu - Kenya
7) Wawakilishi wa Watu wanaoishi na Ulemavu, Wanawake na Watu asili kutoka Mashirika Matatu ya Kijamii
8) Muungano wa Watengezaji Bidhaa wa Kenya
9) Global Compact Network Kenya
10) Kenya National Chamber of Commerce and Industry
11) Muungano wa Sekta ya Kibinafsi nchini Kenya
12) Chama cha Wanasheria nchini Kenya
13) Baraza la Kitaifa la Usimamizi wa Haki
14) Tume ya Kitaifa ya Jinsia na Usawa
15) Shirikisho la Waajiri la Kenya
16) Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira
17) Muungano wa Wafanyakazi Nchini Kenya (COTU)(K)

***Utathmini***

Mpango wa Hatua wa Kitaifa kuhusu Biashara na Haki za Binadamu utakaguliwa baada ya miaka mitano (5).

This publication was published with the support of:

UNDP

THE DANISH INSTITUTE FOR HUMAN RIGHTS

From the People of Japan

***Anwani ya Mawasiliano ya KNCHR***

Orofa ya 1, Jumba la CVS, Barabara ya Lenana/Kasuku Lane

**S.L.P** 74359-00200 , NAIROBI

**Simu:** 0724 256448 SMS: 22359

**Nambari ya simu ya kupiga bila malipo :** 0800720627

**Baruapepe:** haki@knhcr.org

**Wavuti:** www.knhcr.org

KNCHR

Enhancing the realisation of your rights

HARAMBEE

# Toleo la Hatua ya Kitaifa kuhusu Biashara na Haki za Binadamu, Mwongozo Maalum Nambari. 3 wa 2021

## (Toleo Lililorahisishwa)

# LINDA

# HESHIMU

# SULUHISHA

## 1. Je, Toleo la Hatua ya Kitaifa kuhusu Biashara na Haki za Binadamu (NAP -BHR) ni nini?

Mpango wa Hatua wa Kitaifa kuhusu Biashara na Haki za Binadamu ni mkakati thabiti wa serikali wa kulinda dhidi ya dhuluma za haki za binadamu zinazofanywa na biashara, ziwe za kibinafsi au zinazomilikiwa na serikali. NAP-BHR inabainisha ahadi thabiti za serikali za kushughulikia athari mbaya kwa haki za binadamu zinazohusiana na biashara. Hata hivyo, haibuni wajibu wowote mpya ila inataja wajibu uliopo tayari chini ya Katiba ya Kenya 2010, vyombo vya haki za binadamu vya kikanda na kimataifa.

### Maelezo Muhimu

Mpango wa Hatua wa Kitaifa kuhusu Biashara na Haki za Binadamu ni nyaraka ya sera inayojanibisha Kanuni Zinazoongoza Umoja wa Mataifa (UNGP) kuhusu Biashara na Haki za Binadamu. UNGP ziliundwa kupitia wajibu wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, ambaye mwaka wa 2005 alimteua Profesa John Ruggie kama mwakilishi Maalum wa kuchunguza suala la haki za binadamu na ushirika baina ya mataifa mbali mbali pamoja na biashara nyinginezo. Hii ilitokana na ombi la Baraza la Haki za Binadamu. Wajibu wa Mwakilishi Maalum ulikuwa ni kuweka wazi nafasi na majukumu ya serikali, kampuni na washikadau wengine ndani ya upeo wa biashara na haki za binadamu. Profesa John Ruggie, Mwakilishi maalum, alitarajiwa kutoa ripoti ya mwanzo inayowakilisha maoni na mapendekezo ya kuzingatiwa na Baraza la Haki za Binadamu katika Kipindi chake cha 62 mnamo 2006.

Baada ya mashauriano ya kina na viongozi wa biashara, serikali, mashirika ya kijamii, wasomi, asasi za kitaifa za haki za binadamu na washikadau wengine, Profesa Ruggie aliwasilisha Mfumo wa "Linda, Heshimu na Suluhisha". Mfumo huu ulifafanua nguzo tatu, kwa hivyo: Jukumu la serikali la kulinda dhidi ya dhuluma za haki za binadamu, jukumu la Biashara kuheshimu haki za binadamu na, Uwezo wa kufikia suluhu (la mahakama au lisilo la mahakama) endapo kutatokea ukiukaji/dhuluma.




Baada ya kuwasilisha mfumo huu, wajibu wa Profesa Ruggie uliendelezwa na alipewa jukumu la kufanya mfumo huo uweze kufanya kazi pamoja na kuutangaza. Hii ilisababisha ushirikiano zaidi na washikadau hali iliyosababisha kanuni hizo 31 kuwasilishwa kama Kanuni Zinazoongoza Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za Binadamu (UNGP). UNGP zinashughulikia nguzo tatu na kutambua kinachopaswa kufanywa chini ya kila mojawapo. Kanuni hizo zinashughulikia jukumu la serikali la kulinda dhidi ya dhuluma za haki za binadamu zinazofanywa na biashara ziwe za kibinafsi au zinazomilikiwa na serikali, majukumu ambayo biashara zinafaa kuchukua ili kuheshimu haki za binadamu na hatua za suluhu ambazo serikali na biashara zinapaswa kuchukua ili kutatua athari za biashara kwa haki za binadamu. Nchini Kenya, UNGP zinajanibishwa na kutekelezwa kupitia NAP-BHR, Malengo Maalum Nambari. 3.

## 2. Mchakato wa kuunda NAP-BHR

Baada ya kukubalika na Baraza la Haki za Binadamu, serikali ziliombwa kuunda mipango ya hatua ya kitaifa ili kujanibisha na kutekeleza UNGPs katika nchi zao Katika kipindi cha uhakiki wa pili nchini Kenya chini ya kipindi cha Ubia cha Uhakiki mwaka wa 2015, Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa lilipendekeza kwamba Kenya iunde NAP-BHR, pendekezo ambalo lilikubaliwa na Serikali. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Idara ya Haki iliunda hati ya dhana iliyobainisha masuala makuu ya biashara nchini Kenya na kutaka uidhinishaji muhimu ili kuanza kuunda NAP. Mwaka wa 2016, Mwanasheria Mkuu wa Kenya alitoa ahadi kwa umma kwamba Kenya ingeanza kuunda NAP na akaalika washikadau wote kushiriki katika mchakato huo. Idara ya Haki kwa ushirikiano na Tume ya Kitaifa ya Kenya kuhusu Haki za Binadamu iliongoza mchakato wa uundaji.


Kamati Andalizi ya Kitaifa (NSC) ilibuniwa ili kushauri na kushirikisha uundaji wa NAP. Ilikuwa na washikadau wafuatao:

i. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Idara ya Haki
ii. Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu - Kenya
iii. Wizara ya Kawi na Madini
iv. Muungano wa Sekta ya Kibinafsi nchini Kenya
v. Tume ya Haki za Binadamu ya Kenya
vi. Wizara ya Leba na Ulinzi wa Kijamii
vii. Baraza la Magavana
viii. Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu (OHCHR)
ix. Muungano wa Wafanyakazi Nchini (Kenya)
x. Shirikisho la Waajiri la Kenya
xi. Tume ya Kitaifa ya Jinsia na Usawa
xii. United Nations Global Compact

### Malengo ya NAP-BHR

NAP iliundwa ili kutimiza malengo yafuatayo:

i. Kuongoza Serikali katika kutimiza jukumu lake la kulinda watu na jamii dhidi ya dhuluma za haki za binadamu zinazohusiana na biashara kulingana na wajibu wake wa ndani ya nchi na wa kimataifa.
ii. Kuongoza biashara kwa hatua zinazofaa kuchukua ili kutimiza jukumu lao la kuheshimu haki za binadamu katika utendakazi wao
iii. Kuhimiza biashara kufanya uchunguzi wa kina kuhusu haki za binadamu kama hatua thabiti ya kuzuia athari mbaya kwa watu
iv. Kutoa mwongozo wa kuimarisha ufikiaji wa suluhu za Serikali zinazotokana na mahakama na zisizo za mahakama na zile zisizo za serikali kwa waathiriwa wa madhara yanayohusiana na biashara.




Mnamo 2016, NSC ilizindua Tathmini Msingi ya Kitaifa (NBA) ili kutathmini hali ya biashara na haki za binadamu nchini. Msingi huo pia ulitathmini hali ya utekelezaji wa UNGPs na mifumo mingine ya haki za binadamu kuhusiana na biashara.

Baada ya NBA, majadiliano na mazungumzo kuhusu sera yalifanywa na mashirika muhimu ya serikali, biashara, mashirika ya kijamii, jamii na makundi yaliyo hatarini. Majadiliano hayo yalifanywa kote nchini huku vitengo vya zamani vya utawala wa mkoa (mikoa) vikiwa maeneo rahisi ya mikutano. Kadhalika, majadiliano ya kitaifa yalifanyika ili kupata maoni kutoka kwa jamii asili.

### Mada zilizoshughulikiwa kwenye NAP-BHR

NBA na mashauriano yaliyofanywa yalisaidia kutambua masuala ambayo yanayohusu kanda husika na makundi ya washikadau. Baada ya uchanganuzi, yafuatayo yalitambuliwa kama sehemu za mada:

#### a) Ardhi na Maliasili

**Hoja**

- ★ Ukosefu wa maarifa kuhusu muundo uliopo wa fidia na utafutaji wa makazi mbadala kwa ajili ya ununuzi wa hiari na wa lazima wa ardhi
- ★ Ukosefu wa mwongozo kuhusu mashauriano ya jamii katika muktadha wa usimamizi wa maliasili na kusababisha wanajamii kutoshiriki ipasavyo katika kufanya maamuzi
- ★ Ugavi wa ardhi haujafanywa katika baadhi ya maeneo ambapo biashara zinaendeshwa au zinapendekezwa kuendeshwa, hii inafanya kuwa vigumu kufanya maamuzi kuhusu wahusika halali wanaopaswa kufanya ushauriano nao na kupokea fidia
- ★ Sheria ya Uchimbaji Madini, 2016 haijatekelezwa kikamilifu kuhusiana na ugavi wa mapato, hivyo kunyima jamii za ndani zilizoathiriwa na kazi zinazofanywa na kampuni za uchimbaji madini haki na ulinzi chini ya sheria
- ★ Vizuizi vya kitamaduni na kihistoria vinavyokataza wanawake, watu walio wachache na makundi yaliyotengwa kama vile watu asilia kupata ardhi. Vizuizi hivi vinazuia uwezo wa makundi haya kufanya uamuzi na kushiriki katika masuala yanayohusiana na ardhi
- ★ Ukosefu wa manufaa endelevu kwa jamii wenyeji kutokana na maliasili inayotoka kwa ardhi yao licha ya wito wa katiba wa kuwepo usawa katika ugavi wa mafao.

#### b) Uwazi kuhusu Mapato

**Hoja**

- ★ Ufisadi wakati wa kugawa mapato na usimamizi wa mapato ya umma, ufisadi katika mchakato wa utoaji wa leseni kwa biashara, mchakato wa kukusanya kodi na ununuzi wa umma unaodaiwa kufanywa na washikadau wa umma na wa kibinafsi
- ★ Ukosefu wa ufichuzi wa kandarasi hususan zile zilizo na athari kubwa za kiuchumi na kijamii
- ★ Ukosefu wa uwazi katika utawala na usimamizi wa mapato yanayotokana na maliasili ikiwa ni pamoja na shughuli za uchumbaji madini, mafuta na gesi
- ★ Kutokuwepo kwa uwazi kuhusu wamiliki halali wanaostahiki mafao kunasaidia kuficha siri katika kubaini ni nani humiliki na kudhibiiti biashara na kuzuia uwezo wa watekelezaji wa sheria 'kufuata pesa'

#### c) Ulinzi wa Mazingira

**Hoja**

- ★ Uchafuzi wa mazingira kutokana na shughuli za biashara, ikijumuisha kupitia utoaji wa majitaka kwenye mikondo ya maji, uchafuzi wa hewa na kelele na njia mbovu za kutupa taka, bidhaa hatari za sumu. Athari hizi hasi zinahujumu haki za kuwa na mazingira safi na ya kiafya, afya, viwango vinavyofaa vya usafi, maji safi na salama
- ★ Kupoteza viumbe mbalimbali kutokana na uharibifu na kuingiliwa kwa mazingira asili kwa malengo ya kibiashara kunaathiri kwa njia hasi maisha, afya na uwezo wa kufikia maji safi na salama kwa vizazi vya sasa vya vijavyo.

#### d) Haki za leba

**Hoja**

- ★ Dhuluma za kingono zimekithiri na haziripotiwi ipasavyo, wanawake wakiwa ndio waathiriwa zaidi- hofu ya kupoteza kazi ikiwa ni sababu kuu inayofanya dhuluma hizi kutoripotiwa. Isitoshe, Sheria ya Makosa ya Kingono ya 2006 haijatekelezwa ipasavyo
- ★ Kutopatikana kwa likizo kwa kina mama na kina baba. Ingawa sheria inaruhusu na kulinda likizo kwa kina mama na kina baba, si wafanyakazi wote walio katika sekta ya kibinafsi wanaweza kufikia manufaa haya kwa hofu ya kupoteza kazi.
- ★ Kiwango cha chini cha uhamasisho kuhusu haki za leba miongoni mwa wafanyakazi (wengi wakiwa wanawake wanaofanya kazi zenye mapato ya chini au ujuzi wa chini) na waajiri
- ★ Ukosefu wa udhibiti wa mashirika ya ajira kwa ajili ya wafanyakazi ambao ni wahamiaji
- ★ Ukosefu wa takwimu zinazopatikana hadharani zilizopangwa kulingana na mwelekeo wa kingono na hali nyingine hatari zinazoweza kuwa muhimu katika kushughulikia ubaguzi wa kingono na namna nyingine za ubaguzi mahali pa kazi
- ★ Ukosefu wa suluhu kwa waathiriwa wenye malalamiko yanayohusiana na leba yanayotokana na idadi ya juu ya malalamiko yanayohusiana na leba ambayo hayajatatuliwa. Mbinu dhaifu ya utekelezaji, hasa upungufu wa idadi ya maafisa wa ukaguzi wa leba wa serikali na ukosefu wa mbinu zinazofaa za kutatua malalamiko katika kiwango cha utendakazi

#### e) Ufikiaji wa Suluhu

**Hoja**

- ★ Uwezo mdogo wa kufikia mahakama kwa watu wanaoishi mashambani na maeneo ya mbali ambapo hakuna mahakama za kipekee katika miji ya karibu. Upungufu huu ukiongezea gharama ya kupata haki kwa jamii za mtaani
- ★ Licha ya uwezekano wa vikwazo vya uhalifu dhidi ya watendaji na wakurugenzi wa kampuni ambao huenda wamejihusisha katika ukiukaji wa haki mahususi za binadamu ambao pia unahitaji vikwazo vya adhabu ya sheria, kuna kiwango cha chini cha uendeshaji wa mashtaka na hivyo mfumo kukosa kuchukua hatua kama njia ya kuzuia ukiukaji kama huo
- ★ Gharama ya kufungua kesi ni kizingiti kikubwa kwa sehemu kubwa ya wanajamii. Katika baadhi ya mashtaka, kwa mfano, huenda ikawa muhimu kuita wataalamu kama vile wataalamu wa mazingira kutoa ushahidi kuhusu masuala mahususi. Utaalamu kama huo huenda usipatikane kwa jamii au pale unapopatikana, huenda ukawa ghali mno kwa jamii kumudu
- ★ Kumekuwa na matukio ambapo watetezi wa haki za binadamu ambao wameandikisha kesi dhidi ya biashara, hususan malalamiko yanayohusu ardhi na mazingira, wamekabiliwa na matishio ya kifo na namna nyingine za kutishwa ambazo mara nyingi huwa hawapigi ripoti kuzihusu kwa mamlaka. Ukatili huu unaweza kutia woga kwa baadhi ya watu ambao wangependa kutoa malalamiko hivyo kunyima jamii na watu binafsi ulinzi ambao sheria imetoa dhidi ya dhuluma zinazohusiana na biashara
- ★ Uwezo wa majopo ya usimamizi kutoa suluhu isiyo ya mahakama huwa na kikomo kutokana na ukosefu wa wafanyakazi wa kufanya uchunguzi barabara nje ya miji na uwezo wa kiufundi wa kuelewa masuala ibuka na changamano.

**KUMBUKA:** Masuala ya jinsia, makundi yaliyo hatarini kama vile watu wanaoishi na ulemavu, jamii asili na zilizotengwa, wanawake na watoto yalitambuliwa kama masuala mtambuko.

## 3. Hatua za Sera

Taarifa na hatua za sera zimeundwa ili kuitikia wasiwasi unaoibuliwa kupitia nyanja hizo tano za mada na masuala mtambuko. Hatua na taarifa hizi za sera zimeundwa kwa kuangazia nguzo tatu za UNGP.

### Nguzo ya 1: Jukumu la Serikali la Kulinda

Sheria ya kimataifa inaipa serikali jukumu la kulinda dhidi ya dhuluma za haki za binadamu katika maeneo yaliyo chini ya utawala wao. Nguzo ya 1 inaweka wazi wajibu kama huo kuwa unajumuisha kulinda dhidi ya dhuluma za haki za binadamu na wahusika wengine kama vile biashara. Hii inahitaji serikali kuchukua hatua zinazofaa Kuzuia, kuchunguza, kuadhibu na kutatua dhuluma kama hizo. Serikali inafaa kufanya hivi kwa kuweka hatua mwafaka wa sera, sheria, udhibiti na uamuzi.

**NAP inapendekeza Hatua zifuatazo za Sera:**

a) Kuanzisha uhitaji kuhusu Uchunguzi wa Kina wa Haki za Binadamu ili ufanywe kwanza kabla ya kutoa leseni kwa biashara
b) Kuhakikisha kuna mafunzo yanayoendelea kwa wafanyakazi wa mashirika ya serikali wanaohusika katika kuendeleza na kudhibiti biashara kuhusu wajibu wa serikali wa kulinda haki za binadamu na uhusiano na wajibu na utendakazi wao mbalimbali
c) Kuimarisha idara ya uchunguzi wa leba ili kuiwezesha kufanya kazi yake kwa ufanisi
d) Kuunda miongozo kwa ajili kutoa ripoti zisizo za kifedha chini ya Sheria ya Kampuni ya 2015
e) Kuharakisha ugavi na usajili wa ardhi kwa shabaha ya kupata ulinzi kwa wamiliki/watumiaji wa ardhi na jamii hususan katika maeneo yanayonuiwa kufanyiwa miradi mikubwa
f) Kuimarisha mbinu za uangalizi kwa mashirika ya kuajiri watu yanayohusika katika kuajiri Wakenya kwa biashara zilizo ughaibuni. Kuhusiana na hili, serikali itafanya kazi na serikali za nchi wenyeji kuchukua hatua zinazofaa kuhimiza uhamisho salama na sawa wa leba ikijumuisha makubaliano kuhusu uhuru wa kubadilishana taarifa na kudhibiti mashirika ya kuajiri watu kwa njia madhubuti zaidi. Serikali pia itatoa huduma za msaada wa kisheria na kisaikolojia kwa waathiriwa wa dhuluma za leba
g) Kuhamasisha sehemu zinazofaa za umma hususan wanawake na makundi mengine ya watu waliotengwa na walio wachache kuhusu:
    i. Sheria za ardhi ikijumuisha mifumo ya utafutaji wa makazi mbadala na utoaji fidia
    ii. Sheria za leba na haki ya wafanyakazi wahamiaji
    iii. Sheria na viwango vya mazingira
h) Kuunda miongozo ya kiutaratibu itakayotumiwa na biashara, watu binafsi na jamii katika maafikiano yao kuhusu ufikiaji na ununuzi wa ardhi. Miongozo hii itahakikisha na kulinda kushiriki kwa wanawake, watu wanaoishi na ulemavu, vijana, watoto na makundi mengine ya watu waliotengwa.
i) Kufanya kazi na washikadau kuunda sera ya usimamizi wa mapato yanayotokana na maliasili na mfumo wa udhibiti kwa ajili ya kudhibiti na kusimamia mapato yanayotokana na maliasili yanayolipwa kwa jamii wenyeji. Mfumo huu unapaswa kutaka kuhimiza usawa, ujumuishaji na uamuzi unaofanywa na jamii na utajumuisha mafunzo ili kuboresha uwezo wa jamii kudhibiti mambo yao. Pia utatumika kutoa mwongozo wa utekelezaji wa mapato yanayotokana na uchimbaji madini kama ilivyobainishwa kwenye Sheria ya Uchimbaji Madini ya 2016.
j) Kukamilisha kuunda kanuni za Sheria ya ufikiaji wa taarifa ili kuwezesha ufichuzi wa kandarasi, ikijumuisha zile ambazo zina athari kubwa ya kiuchumi na kijamii nchini na kujiunga na Mpango wa Uwazi wa Sekta ya Uchimbaji (EITI) ili kuwezesha uwazi wa mapato.
k) Kuimarisha matumizi ya ununuzi wa umma ili kuendeleza haki za binadamu. Hii itahusisha kukaguliwa kwa sera, sheria na viwango vilivyopo vya ununuzi wa umma na athari zao kuhusiana na wajibu wa serikali wa kulinda haki za binadamu ikijumuisha haki za wanawake kama sehemu ya kigezo
l) Kukagua makubaliano ya sasa ya kutangaza biashara na uwekezaji na kuzifanya ziambatane na Katiba na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu ili kuhakikisha hayatumiki kuwezesha mitiririko haramu ya kifedha na biashara kuepuka kulipa kodi.

### Nguzo ya 2: Jukumu la Kiushirika ili kuheshimu Haki za Binadamu

Nguzo hii inasema kwamba biashara zinapaswa kuheshimu haki za binadamu kila mahali zinapoendeshwa. Heshima hii inapatikana kwa kuhakikisha kwamba zinaepuka kudhulumu haki za wengine na pale ambapo madhara tayari yametokea, zinapaswa kuchukua hatua za kuyasuluhisha. Biashara zinafaa kutumia uchunguzi wa kina wa haki za binadamu kama zana msingi ya kuhakikisha kwamba zinatumbua hatari za haki za binadamu zinazoletwa na shughuli zao, zichukue hatua za kuziepuka au kuzitatua na pale ambapo madhara hayo yametokea, zihakikishe kwamba waathiriwa wanaweza kufikia suluhu zinazofaa.

**Hatua za Sera**

a) Mafunzo: Serikali inafaa kuunda na kusambaza mwongozo kwa biashara na jukumu lao la kuheshimu haki za binadamu na kutekeleza jukumu hili katika muktadha wa Kenya, ikijumuisha athari ya shughuli zao kwa mazingira, jinsia, watetezi wa haki za binadamu, watu walio wachache, watu wanaoishi na ulemavu, jamii zilizotengwa na makundi mengine ya watu walio hatarini ili kuendeleza matendo ya leba ya kuwajibika na ujumuishaji
b) Ahadi za Sera za Haki za Binadamu- Serikali inapaswa:
    i. Kufanya iwe sharti kwa biashara zote kutekeleza sera za haki za binadamu, ikijumuisha kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba shughuli zao zinaheshimu haki za binadamu, ikijumuisha kwa kutoa ufikiaji wa suluhu kwa dhuluma za haki za binadamu
    ii. Kuhimiza mashirika ya kuajiri watu kutoa msaada wowote unaohitajika wa uhamiaji, wa kisheria na kisaikolojia kwa wafanyakazi wahamiaji ambao wamepitia au kudhulumiwa wakiwa ng'ambo
    iii. Kutekeleza utiifu wa viwango vya haki za binadamu na Mashirika Yanayomilikiwa na Serikali na biashara nyingine ambazo zinapokea mkopo wa kuuza bidhaa katika nchi za nje na msaada wa serikali ikijumuisha kutoa uwezo wa kufikia suluhu kwa ukiukaji wa haki za binadamu